**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

# 03 MAARIFA YA JAMII

**Muda: Saa 1:30** **Alhamisi, 21 Novemba 2019**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu A na B zenye jumla ya maswali **manne (4).**
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

## SEHEMU A: (Alama 28)

**1.** Jibu kipengele cha (i) – (viii) kwa kuchagua **herufi ya jibu sahihi** na kuiandika kwenye kisanduku.

i. Bwana Juma huishi na mkewe, watoto wawili na dada yake. Hii ni aina gani ya familia?
A. Familia ya awali C. Familia pana.
B. Familia ya mzazi mmoja. D. Familia ya makubaliano. [ ]

ii. Migogoro kati ya wakulima na wafugaji husababishwa na ________
A. Vyama vingi vya siasa C. Uhaba wa mifugo na mazao.
B. Uhaba wa ardhi D. Kupungua kwa wafugaji. [ ]

iii. Dada wa baba yangu huitwa?
A Mama B Bibi. C Shangazi. D Dada. [ ]

iv. Kwanini tunawakumbuka viongozi wetu wakuu wa nchi ya Tanzania wa zamani?
A. Walituletea amani na umoja C. Walituletea utawala wa kigeni.
B. Walituletea fedha za kutosha D. Walituletea mifarakano [ ]

v. Ni sera gani kati ya hizi iliasisiwa na Rais wa zamani Ali Hassan Mwinyi?
A. Ujamaa na Kujitegemea C. Elimu bure kwa wote
B. Soko huria. D. Ubinafsishaji. [ ]

vi. Zifuatazo ni hasara za uhusiano mbaya wa wanafunzi shuleni, ***isipokuwa:***
A. Kuchukia masomo C. Kutengeneza maadui shuleni.
B. Kutoweka kwa amani shuleni. D. Kukuza mshikamano shuleni

vii. Ni kundi lipi la jamii za Kitanzania bado linaendeleza mfumo wa ujima?
A. Wandorobo, Wasandawe, na Wamakonde.
B. Wamasai, Wasandawe, na Wafipa.
C. Wahadzabe, Wandorobo, na Wakurya.
D. Wandorobo, Wasandawe na Wahadzabe. [ ]

viii. Moja ya faida tunayoipata kwa kucheza ngoma za utamaduni ni
A. Kuendeleza utandawazi C. Kukuza mila na desturi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

B. Kuwaburudisha wazungu D. Kudumisha lugha za kigeni. [ ]

**2.** Jibu kipengele cha (i) hadi (vi) kwa kuoanisha maelezo ya fursa mbalimbali kutoka **Fungu A,** na aina husika ya fursa husika kutoka **Fungu B**.

| Na. | Fungu A | Herufi | Fungu B |
|---|---|---|---|
| i. | Fursa zilizopo kwenye maeneo yenye mbuga za wanyama. | | A. Kilimo<br>B. Mbao<br>C. Madini<br>D. Uashi<br>E. Ufundi<br>F. Ufugaji<br>G. Utalii<br>H. Uvuvi |
| ii. | Fursa zilizopo maeneo yenye misitu. | | |
| iii. | Fursa zilizopo maeneo yenye rutuba na mvua nyingi. | | |
| iv. | Fursa zilizopo maeneo yenye uwanda wa nyasi. | | |
| v. | Fursa zilizopo maeneo yenye mito, maziwa na bahari. | | |

## SEHEMU B: Maswali ya Majibu Mafupi

**3.** Soma kifungu cha habari na kisha jibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho.


*Hali ya joto au baridi ya sehemu au kitu huitwa jotoridi. Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa kipimajoto. Chanzo cha cha joto ni jua. Kunapokuwa na joto kali tunasema jotoridi liko juu lakini kunapokuwa na baridi tunasema joto liko chini. Kunapokuwa na baridi tunashauriwa kuvaa nguo nzito kama sweta na jaketi. Wakati wa joto kali tunavaa nguo nyepesi au nguo za pamba. Hali ya joto husababisha mito na mabwawa kukauka.*

**Maswali:**

i. Hali ya joto au baridi ya mahali huitwaje? ___________
ii. Mavazi gani huvaliwa wakati wa baridi? ____________
iii. Ni katika hali gani jotoridi huwa juu? ______________
iv. Kifaa kinachotumika kupima jotoridi huitwa? ________
v. Chanzo cha jotoo ni nini? _________________________
vi. Mito na mabwawa hukauka wakati gani? ___________
vii. Nguo nyepesi na za pamba huvaliwa wakati gani?

**4.** Soma kwa makini ramani ya kijiji cha Mtakuja uliyopewa, na kisha jibu vipengele vilivyoulizwa kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizo wazi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org




**Maswali:**

i. Kuna madaraja mangapi katika ramani? __________
ii. Kuna milima mingapi katika ramani? ____________
iii. Kuna visima vingapi katika ramani? _____________
iv. Mto B unamwaga wapi maji yake? ______________


Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org